

## Ni nani tunaweza kusaidia

Huduma za Relationships Australia WA zinapatikana kwa watu wa asili zote za kitamaduni, muundo wote wa familia, jinsia yote na mwelekeo wote wa kijinsia.

Tunatoa msaada kwa:

- wapenzi na familia
- watu binafsi
- watoto na vijana
- bibi na babu na walezi
- wazee na familia zao
- Watu wa Asili na wa Visiwa vya Torres Strait
- wakimbizi na waliwasili kwa hisani
- watu wanaopita vurugu vya nyumbani au familia
- watu wenye matatizo ya afya ya akili
- wapenzi wa jinsia moja
- mashirika ya kitaalamu
- vikundi vya jamii

## Maeneo yetu katika WA

Tuna maeneo katika jimbo lote. Hayo yanajumuisha:

Albany	Kwinana
Bunbury	Mandurah
Busselton	Midland
Fremantle	Northam
Gosnells	South Hedland
Joondalup	West Leederville

## Wasiliana nasi

Kujifunza zaidi:

piga simu **1300 364 277**

tembelea [www.relationshipswa.org.au](http://www.relationshipswa.org.au)

tuma barua pepe  
[info@relationshipswa.org.au](mailto:info@relationshipswa.org.au)

fuata kwetu kwa Twitter [@RelationshipsWA](https://twitter.com/RelationshipsWA)

au onyesha alama ya kutupenda  
kwenye Facebook [@RelationshipsWA](https://www.facebook.com/RelationshipsWA)

*Relationships Australia*  
WESTERN AUSTRALIA

Version 1 - May 2021



**Sisi ni nani  
Kile  
tunachofanya**

*Relationships Australia*  
WESTERN AUSTRALIA

Swahili - Kiswahili

## Sisi ni nani

Kwa muda wa zaidi ya miaka 60 Relationships Australia WA imekuwa inatoa huduma za msaada wa uhusiano kwa watu binafsi, wapenzi, familia na jamii.

Sisi ni shirika lisilo la faida la huduma ya jamii bila ushirika wowote wa kidini. Tunabadilisha huduma zetu kulingana na mahitaji yako, kukusaidia wakati wa changamoto na mabadiliko.

## Jinsi tunavyoweza kusaidia

Kwa kuwa na programu na huduma mbalimbali tunaweza kusaidia katika maswala au mada mbalimbali, ikijumuisha:

- unyumba na mahusiano
- kujenga mahusiano
- kuachana na kuanza tena
- uzazi na uzazi wa kambo
- mimba isiyopangwa
- mizozo ya familia
- upatanishi na ushauri mahali pa kazi
- dawa za kulevya na pombe
- hasira
- vurugu vya nyumbani na vya familia
- kufiwa na huzuni
- kuwasiliana
- usawa wa kitamaduni
- afya ya kiakili (mental health)

## Kile tunachofanya

Miradi na huduma zetu zinajumuisha:

### Ushauri nasaha

Nafasi za kujadiliana maswala yanayosababisha wasiwasi katika mazingira yenye msaada, heshima na usiri. Ushauri nasaha ni kwa watu binafsi, wapenzi, au familia.

### Upatanishi

Tunatumia wapatanishi wenye idhini na watendaji wa kusuluhisha mizozo ya familia kusaidia watu kutatua mizozo. Wawezeshaji wana asili anuwai ikiwa ni pamoja na ushauri, saikolojia, kazi ya ustawi wa jamii, tiba ya familia, sheria na usimamizi.

### Elimu ya Jamii

Chagua kutoka kwa anuwai ya semina za usiku mmoja na kozi ndefu kwa watu binafsi, wanandoa na familia.

### Mensplace (Mahali pa Wanaume)

Huduma ya kusaidia wanaume kushughulikia maswala ya uhusiano na familia.

### Maendeleo ya Kitaalamu

Tunatoa programu mbalimbali inayolenga kukusaidia katika mahali pa kazi.

### Huduma za Mawasiliano za Watoto

Kusaidia wazazi kukuza njia zao zenyewe za kusimamia mipangilio ya mawasiliano inayokuwa kwa hali bora ya watoto wao.

### Huduma za Watu wa Asili

Kwa kuongezea huduma zetu za jumla, pia tunatoa programu kadhaa haswa kwa watu wa Asili na wa Visiwa vya Torres Strait. Hii inajumuisha Huduma za Morrditj ya Kujadili na Djinda.

## Huduma za Vurugu za Nyumbani na za Familia

Programu hizi za kikundi za bure ni za wanawake, vijana, watoto au wanaume ambao wamepata au kufanya matumizi mabaya katika familia zao au katika mahusiano yao.

### Tafuta na Ungana

Huduma ya kusaidia kuboresha maisha ya Waaustralia Waliosahaulika na Wahamiaji wa Watoto wa Zamani.

## Huduma ya Msaada wa Kuchukuliwa kulelewa kwa Lazima

Huduma kwa mtu yeyote ambaye ameathiriwa na kulelewa kwa lazima.

### Huduma ya Msaada wa Ukarabati

Inasaidia watu ambao wanafikiria juu ya kutuma ombi kwa Mpango wa Kitaifa wa Ukarabati.

### Ushauri nasaha na Msaada

Huduma hii ni kwa watu walioathiriwa na Disability Royal Commission (Tume ya Kitaifa ya Ulemavu).

### Msaada kwa Wazee

Huduma hizi zinalenga kusaidia wazee na familia zao kukuza na kudumisha mahusiano mazuri, yenye afya ambayo yanakuzwa na kuthaminiwa.

### Programu ya Msaada wa Wafanyakazi

Programu ya Msaada wa Wafanyakazi (Employees Assistance Program -EAP) ni huduma mbalimbali za kusaidia wafanyakazi na waajiri katika kushughulika na maswala ya kibinafsi na ya kazi ambayo yanaweza kuathiri ustawi wa mtu, utendaji wa kazi na ari ya shirika.

